



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO AWAMU YA PILI (ASDP II)**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO  
AWAMU YA PILI (ASDP II) KWA KIPINDI CHA MWAKA 2022/2023**

**OKTOBA, 2023**

## YALIYOMO

<b>MAJEDWALI</b>	<b>iv</b>
<b>VIELELEZO</b>	<b>vi</b>
<b>VIAMBATISHO</b>	<b>vi</b>
<b>AKRONIMI</b>	<b>viii</b>
<b>DIBAJI</b>	<b>xi</b>
<b>1.0. UTANGULIZI</b>	<b>1</b>
<b>2.0. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2022-2023</b>	<b>2</b>
<b>2.1. Eneo Kuu la Kwanza: Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Ardhi na Maji na Ardhi</b>	<b>5</b>
2.1.1 Mpango wa Matumizi ya ardhi na usimamizi wa mabwawa	6
2.1.2 Maendeleo ya Miundombinu ya Umwagiliaji	6
2.1.3 Kuendeleza vyanzo vya maji kwa ajili ya mifugo na Uvuvi	7
<b>2.2. Eneo Kuu la Pili: Kuongeza Tija na Faida Katika Kilimo, Mifugo na Uvuvi</b>	<b>7</b>
2.2.1 Kuimarisha huduma za ugani, mafunzo na uendelezaji wa huduma za taarifa	8
2.2.2 Utafiti na maendeleo	8
2.2.3 Upatikanaji bora wa pembejeo na huduma za afya ya mazao, mifugo na uvuvi	8
2.2.4 Kuimarisha na kukuza uchumi wa kilimo (mazao, mifugo na Uvuvi)	9
<b>2.3. Eneo Kuu la Tatu: Biashara na Kuongeza thamani ya mazao</b>	<b>10</b>
2.3.1 Kuendeleza upatikanaji wa soko kwa bidhaa zote za kipaumbele	10
2.3.2 Maendeleo ya biashara za kilimo, Miundombinu ya kuongeza thamani na usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo na Uvuvi	11
<b>2.4. Eneo kuu la Nne: Uwezesaji wa Sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini</b>	<b>11</b>
2.4.1 Sera na Mfumo wa udhibiti na Maendeleo ya Mazingira ya Biashara	12
2.4.2 Kuimarisha uwezo wa taasisi na wa kiufundi wa wazalishaji wadogo waliopo na wapya, biashara na vikundi vya wakulima wa usindikaji na vyama vya ushirika	12
2.4.3 Kuboresha na kuimarisha uratibu kati ya Wizara za Kisekta na Wadau	13
2.4.4 Kuendeleza mfumo wa ufuatiliaji na tathmini katika sekta ya kilimo	13
2.4.5 Upatikanaji wa mikopo, huduma za kifedha na bima	14
<b>3.0. USHIRIKI WA WASHIRIKA WA MAENDELEO:</b>	<b>15</b>
<b>4.0. USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI</b>	<b>17</b>
<b>5.0. MAFANIKIO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU</b>	<b>19</b>
<b>5.1. Mafanikio kwenye Malengo ya Muda Mrefu</b>	<b>20</b>
<b>5.2. Mafanikio kwenye Malengo ya Muda Kati</b>	<b>21</b>
5.2.1 Mafanikio ya Muda wa Kati Eneo la Matumizi Endelevu ya Ardhi na Maji	22
5.2.2 Mafanikio ya Muda wa Kati Eneo la Kuongeza Tija na Faida Katika Kilimo	23
5.2.3 Mafanikio ya Muda wa Kati Eneo la Biashara na Kuongeza Thamani	24

5.2.4.	Mafanikio ya Muda wa Kati Eneo Uwezeshaji, Uratibu, Ufutiliaji na Tathmini	25
<b>5.3.</b>	<b>MAFANIKIO YA MUDA MFUPI KATIKA UTEKELEZAJI WA ASDP II</b>	<b>25</b>
5.3.1.	Mafanikio ya Muda Mfupi Eneo la Matumizi Endelevu ya Ardhi na Maji	26
5.3.2.	Mafanikio ya Muda Mfupi Eneo Kuu la Biashara na Kuongeza Thamani	29
5.3.3.	Mafanikio ya Muda Mfupi Eneo Kuu la Uwezeshaji, Uratibu, Ufutiliaji na Tathmini	29
<b>6.0.</b>	<b>CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI PROGRAMU NA HATUA ZA UTATUZI</b>	<b>30</b>
6.1.	Changamoto kwenye Eneo Kuu la Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Maji	31
6.2.	Changamoto kwenye Eneo Kuu la Kuongeza Tija na Faida Kwenye Kilimo	32
6.3.	Changamoto kwenye Eneo Kuu la Biashara na Kuongeza Thamani	34
6.4.	Changamoto kwenye Eneo Kuu la Uwezeshaji wa Sekta, Uratibu, Ufutiliaji na Tathmini	34
<b>7.0.</b>	<b>HITIMISHO</b>	<b>37</b>

## **MAJEDWALI**

Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023 ya ASDP II Wizara za Kisekta.....	2
Jedwali Na. 2: Utekelezaji wa Bajeti ya ASDP II Mwaka 2022/2023 Wizara/Taasisi za Kisekta .	3
Jedwali Na. 3: Kiwango cha utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2022/2023.....	5
Jedwali Na.4: Utekelezaji wa kazi kwenye Eneo Kuu la Kwanza Mwaka 2021/2022.....	5
Jedwali Na.5: Utekelezaji wa kazi kwenye Eneo Kuu la Pili Mwaka 2022/2023 .....	7
Jedwali Na.6: Utekelezaji wa kazi kwenye Eneo Kuu la Tatu Mwaka 2022/2023 .....	10
Jedwali Na.7: Utekelezaji wa kazi kwenye Eneo Kuu la Nne Mwaka 2021/2022 .....	12
Jedwali Na. 8: Kiasi cha Mkopo uliotolewa na Taasisi za Kifedha* .....	14
Jedwali Na. 9: Miradi ya moja kwa moja ya Washirika wa Maendeleo Mwaka 2022.....	16
Jedwali Na. 10: Mlinganyo wa uzalishaji wa baadhi ya mazao katika Sekta Binafsi .....	17
Jedwali Na. 11: Uwekezaji Sekta Binafsi kwa muktadha wa mikopo ya kibenki.....	18
Jedwali Na. 12: Mlinganisho wa Mafanikio mwaka 2022/2023.....	19
Jedwali Na. 13: Mlinganisho wa Mafanikio mwaka 2022/2023.....	20
Jedwali Na 14. Mazao yaliyouzwa zaidi nje ya nchi .....	21
Jedwali Na. 15: Ufikiwaji wa mafanikio ya muda wa kati kwa maeneo na sekta .....	22
Jedwali Na. 16: Mafanikio mahsus ya muda wa kati .....	22
Jedwali Na. 17: Uzalishaji wa mazao ya kipaumbele kwa mwaka.....	23
Jedwali Na. 18: Ukuaji wa matumizi ya mbinu na teknolojia bora za kilimo .....	23
Jedwali Na. 19: Mafanikio ya muda wa kati kwenye biashara na kuongeza thamani.....	25
Jedwali Na. 20: Mafanikio ya muda mfupi kwa maeneo na sekta .....	26
Jedwali Na. 21: Mafanikio ya Muda Mfupi Eneo Kuu la Matumizi Endelevu ya Ardhi na Maji... ..	27
Jedwali Na. 22: Mafanikio ya Muda Mfupi Eneo Kuu la Kuongeza Tija na Faida Kwenye Kilimo .....	28
Jedwali Na. 23: Mafanikio ya Muda Mfupi Eneo Kuu la Biashara na Kuongeza Thamani.....	29
Jedwali Na. 24: Mafanikio ya Muda Mfupi Uwezeshaji, Uratibu, Tathmini na Ufuatiliaji .....	30
Jedwali Na. 25: Changamoto katika utekelezaji Eneo Kuu la Usimamizi wa Matumizi Endelevu wa Ardhi na Maji.....	32

Jedwali Na. 26: Changamoto za Utekelezaji Eneo Kuu la Kuongeza Tija na Faida kwenye Kilimo, Mifugo na Uvubi.....	33
Jedwali Na. 28: Changamoto za Utekelezaji katika Uwezeshaji wa Sekta Uratibu, Ufutiliaji na Tathmini. ....	35

## **VIELELEZO**

Kielelezo Na. 1: Utekelezaji wa Bajeti ya ASDP II .....	4
Kielelezo Na. 2: Kiwango cha Fedha za Nje kwenye Bajeti ya Sekta ya Kilimo.....	15
Kielelezo Na. 3: Ukuaji wa Sekta ya Kilimo.....	20
Kielelezo Na. 5: Utekelezaji wa Bajeti ya ASDP II Mwaka 2018/2019-2022/2023 .....	31
Kielelezo Na. 6: Muundo wa Uratibu ASDP II .....	36

## **VIAMBATISHO**

Kiambatisho Na.1: Mchanganuo wa Gharama za ASDP II .....	38
Kiambatisho Na. 2: Mchanganuo wa Fedha Zilizoidhinishwa .....	39

Kiambatisho Na. 3: Mchanganuo wa Fedha Zilizotolewa .....	40
Kiambatisho Na. 4: Mchanganuo wa Fedha Zilizotumika.....	41
Kiambatisho Na. 5: Mchanganuo wa Bajeti ya ASDP II .....	42
Kiambatisho 6: Wasifu wa Utekelezaji Gharama za Miradi Elekezi ya ASDP II .....	43
Kiambatisho Na. 7: Utekelezaji wa miradi/kazi kwa Eneo na Sekta.....	<b>Error! Bookmark not defined.</b>
Kiambatisho Na. 8: Utekelezaji wa miradi kwa Wizara na Taasisi.....	45
Kiambatisho Na. 9: Utekelezaji wa Programu Wizara/Taasisi za Kisekta .....	46
Kiambatisho Na. 10: Utekelezaji wa Programu Sekretarieti za Mikoa .....	109
Kiambatisho Na. 11: Utekelezaji wa Programu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa .....	150
Kiambatisho Na. 12: Ushiriki wa Washirika wa Maendeleo.....	222
Kiambatisho Na. 13: Idadi na wasifu wa viashiria kwenye jedwali la matokeo .....	243
Kiambatisho Na. 14: Mafanikio Sekta ya Kilimo – Mazao .....	245
Kiambatisho Na. 15: Mafanikio Sekta ya Kilimo-Mifugo.....	246
Kiambatisho Na. 16: Mafanikio Sekta ya Kilmo - Uvumi.....	247
Kiambatisho Na. 17: Mafanikio Sekta ya Kilimo - Mtambuka .....	248
Kiambatisho Na. 18: Jedwali la Matokeo ASDP II .....	249

## AKRONIMI

ACT	Agricultural Council of Tanzania
AFDP	Agriculture and Fisheries Development Programme
AGITF	Agricultural Inputs Trust Fund
AMCOS	Agricultural Marketing Co-operative Societies
AR4D	Agricultural Research for Development
ARDS	Agricultural Routine Data System
ASDP II	Agricultural Sector Development Programme Phase II
ASLMs	Agricultural Sector Lead Ministries
BMGF	Bill & Melinda Gates Foundation
BMU	Beach Management Unit
CC	City Council
CGIAR	Consortium Group International Agricultural Research
CIAT	The International Center for Tropical Agriculture
CIP	The International Potato Center
CPB	Cereals and Other Produce Board of Tanzania
CPU	Central Pulping Unit
CVL	Village land certificates
DADPs	District Agricultural Development Plans
DANIDA	Danish International Development Agency
DASIP	District Agricultural Sector Investment Project
DC	District Council
DPs	Development Partners
EACOP	The East African Crude Oil Pipeline
EFTA	Equity For Tanzania Limited
ENABEL	The development agency of Belgium's federal government
ERPP	Expanded Rice Production Project
ESIA	Environmental and Social Impact Assessment
ESMP	Environmental and Social Management Plan
EU	European Union
FAO	Food and Agriculture Organization
GDP	Gross Domestic Product
GMO	Genetically modified organism
HORTI	Horticultural Research & Training Institute
ICRISAT	The International Crops Research Institute for the Semi-Arid Tropics
IFAD	The International Fund for Agricultural Development
IITA	International Institute of Tropical Agriculture
ILMIS	The Land Management Information System
IMF	International Monetary Fund
IRRI	International Rice Research Institute
JICA	Japan International Cooperation Agency
JIRCAS	Japan International Research Center for Agricultural Sciences
JKT	Jeshi la Kujenga Taifa
JNHP	Julius Nyerere Hydropower Project
KATC	Kilimanjaro Agricultural Training Centre

KATRIN	Kilombero Agricultural Training and Research Institute
KFC	Kibaigwa Flour Supplies
LGAs	Locl Government Authorities
LITA	Livestock Training Agency
LMU	Livestock Multiplication Unit
MATI	Ministry of Agriculture Training Institute
MC	Municipal Council
MIT	Ministry of Industry and Trade
MLF	Ministry of Livestock and Fisheries
MLHHS	Ministry of Lands, Housing and Human Settlement Development
MoA	Ministry of Agriculture
MoF	Ministry of Finance
NBC	National Bank of Commerce
NBS	National Bureau of Statistics
NEMC	National Environment Management Council
NFRA	National Food Reserve Agency
NIC	National Insurance Corporation
NIRC	National Irrigation Commission
NLUPC	National Land Use Planning Commission
NMB	National Microfinance Bank
NORAD	Norwegian Agency for Development Cooperation
PO-RALG	President's Office Regional Administration and Local Government
QDS	Quality Declared Seed
RS	Regional Secretariet
SAGCOT	Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania
SCAJ	Specialty Coffee Association of Japan
SGR	Tanzania Standard Gauge Railway
SIDA	Swedish International Development Cooperation Agency
SIDO	Small Industries Development Organization
SMEs	Small and medium-sized enterprises
TACRI	Tanzania Coffee Research Institute
TADB	Tanzania Agricultural Development Bank
TAFICO	Tanzania Fishing Corporation
TAFIRI	Tanzania Fisheries Research Institute
TAFSIP	Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan
TAHA	Tanzania Horticultural Association
TAISP	Tanzania Agricultural Input Support Project
TANEPS	Tanzania National Electronic Procurement System
TANIPAC	Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination
TANSHEP	Tanzania Smallholder Horticulture Empowerment and Promotion
TARI	Tanzania Agricultural Research Institute
TARURA	The Rural and Urban Roads Agency
TBD	To be determined
TBL	Tanzania Breweries Limited
TC	Town Council
TCD	Technical Committee of Directors

TDV	Tanzania Development Vision
TEHAMA	Teknolijia ya Habari na Mawasiliano
TIB	Tanzania Investment Bank
TIRDO	Tanzania Industrial Research and Development Organization
TORITA	Tobacco Research Institute of Tanzania
TOSCI	Tanzania Official Seed Certification Institute
TPRI	Tropical Pesticides Research Institute
TPSF	Tanzania Private Sector Foundation
TRIT	Tea Research Institute of Tanzania
TSHTDA	Tanzania Smallholder Tea Development Agency
TVLA	Tanzania Veterinary Laboratory Agency
UN WOMEN	The United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women
UNDP	United Nations Development Programme
UNIDO	United Nations Industrial Development Organization
USAID	United States Agency for International Development
USD	United States dollar
UVIKO	Ugonjwa wa Virusi vya Korona
WARC	Ward Resource Centres
WB	World Bank
WFP	World Food Programme
WRRB	Warehouse Receipts Regulatory Board

## DIBAJI

Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) ni programu mwamvuli katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi nchini. ASDP II inajumuisha programu, miradi na kazi mbalimbali zenye ni kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo (kilimo-mazao, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na tija, kukifanya kilimo kiwe cha kibashara zaidi na kuongeza pato la wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha yao, usalama wa chakula na lishe. ASDP II ni Programu ya miaka kumi na imeanza kutekelezwa mwaka 2018/2019 na ina makuu manne ambayo ni: (i) Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Maji na Ardhi (UMA), (ii) Kuongeza Tija na Faida katika Kilimo, Mifugo na Uvuvi (KFK), (iii) Biashara na Kuongeza thamani ya Mazao (BTM) na (iv) Kuiwezesha Sekta katika Uratibu, Ufuatiliaji na Tathimini (SUT). Programu inatekelezwa na Serikali, Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi.

Tathmini ya utekelezaji wa ASDP II kwa mwaka 2022/2023 imefanyika ili pamoja na mambo mengine, kujua hatua iliyofikiwa kiutekelezaji kwa mwaka husika na akisi ya mafanikio kwa miaka mitano tangu ilipoanza kutekelezwa mwaka 2018/2019. Baadhi ya matokeo makuu yanaonesha kuwa Uwekezaji wa Serikali umeongezeka kutoka Sh. 445,587,907,297 katika mwaka 2019/2020 hadi kufikia Sh. 1,499,951,628,257 katika mwaka 2022/2023. Kiwango cha usaidizi wa fedha za nje kwenye bajeti umepungua kutoka 15% hadi kufikia 11% katika kipindi hicho. Ufadhilli wa miradi ya moja kwa moja ilikadirisha kuwa Sh. 314,502,359,205 kwa mwaka 2022/2023. Aidha, uwekezaji wa Sekta Binafsi katika minyororo ya thamani ya mazao anuai umeongezeka kutoka Sh. 53,249,400,000 katika mwaka 2018/2019 hadi kufikia Sh. 1,807,481,862,772 katika mwaka 2022/2023.

Utendaji jumuishi wa programu katika maeneo yote makuu unaonesha kuwa utekelezaji umefanikiwa kwa 49%. Matokeo mapana ya mafanikio ya programu yalikuwa 57% ambayo yamechangiwa na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi katika mazao ya nyama, samaki, korosho, kahawa na mwani huku uagizaji wa nyama ya ng'ombe na maziwa kutoka nje ya nchi ukipungua. Mafanikio katika kufikia malengo kwenye sekta ndogo ya Mifugo yalikuwa asilimia 74, yalikifuatiwa na sekta mtambuka (53%), Uvuvi (51%) na mazao (34%). Mafanikio kwenye UMA pamoja na mambo mengine ulichangiwa na ongezeko la ujenzi wa skimu za umwagiliaji, vizimba vya kufugia samaki, mabwawa ya kunyweshea wanyama na kupungua kwa migogoro ya ardhi. Matokeo chanya upande wa KFK umetokana kuongezeka kwa tija kwenye uzalishaji wa mazao ya chakula kama vile mahindi, maharage, nyama na mazao ya maziwa; matumizi ya mbolea na mashine rahisi za shambani kama vile *power tillers* na *spraying pumps*. Maendeleo ya Miundombinu ya masoko yameongeza utendaji wa mnyororo wa thamani wa mazao. Vilevile, kulikuwa na udhibiti bora wa upotevu wa mazao baada ya mavuno katika mazao ya mahindi, alizeti, nyanya, mihogo na mazao ya maziwa wakati tofauti ya bei ya shamba na ya sokoni ilipungua kama mahindi, mpunga na maharage.

Tathmini kwenye Eneo Kuu la Uwezeshaji wa Sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini unaonesha kuongezeka kwa uwezeshwaji wa Sekta hususan kuongezeka kwa Bajeti, mikopo inayotolewa kwa sekta na matumizi ya mfumo wa takwimu. Hata hivyo, uthabiti wa mafanikio kwenye eneo hili kuu umetokana na viashiria chini ya wastani yumkini kwa sababu ya ushirikishwaji hafifu wa wadau. Hivyo, uimarishaji wa uratibu wa sekta ni muhimu kwa matokeo chanya na jumuishi.

## **1.0. UTANGULIZI**

Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) imeanza kutekelezwa kuanzia mwaka 2018/2019 kwa kipindi cha miaka mitano ya kwanza hadi mwaka 2022/2023 ikiwa na lengo la kuleta mageuzi ya Sekta ya Kilimo (kilimo, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na tija, kufanya kilimo kiwe cha kibiashara zaidi na kuongeza pato la wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha yao, uhakika wa usalama wa chakula na lishe na kuchangia katika pato la Taifa.

Fedha zilizoainishwa kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Programu kwa miaka mitano ni shilingi **13,819,077,626,470** ambapo katika mwaka wa tano wa utekelezaji ziliainishwa kiasi cha shilingi **3,230,251,114,821**. Fedha hizo zimepangwa kutumika katika maeneo makuu manne ya programu ambayo ni Matumizi Endelevu ya Ardhi na Maji (asilimia 15); Kuongeza tija na Faida katika Kilimo (asilimia 58); Biashara na Kuongeza Thamani (asilimia 26) na Uwezeshaji wa Sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini (asilimia 1). Programu inatekelezwa kwa pamoja na Serikali, Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi.

Kwa upande wa Serikali, Programu hii inatekelezwa na Wizara sita za sekta ya kilimo (ASLMs) ambazo ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na Wizara ya Maji. Vilevile, programu inatekelezwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Magereza na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia Jeshi la Kujenga Taifa.

Katika mwaka 2022/2023 Wizara za sekta ya kilimo, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilidhinishwa jumla ya Shilingi **1,499,951,628,257**. Aidha, katika fedha zilizoidhinishwa, Shilingi **1,336,789,471,560** sawa na asilimia 89 ni fedha za ndani na Shilingi **163,162,156,697** sawa na asilimia 11 ni fedha za nje (Jedwali Na. 1 na Kiambatisho Na. 1-3).

Aidha, kiasi cha Shilingi **314,502,359,204.94** ziliwekezwa kupitia miradi ya moja kwa moja inayotekeliza na kufadhiliwa na Washirika wa Maendeleo (DPs) kwa mwaka 2022/2023. Usaidizi wa DPs kwenye bajeti na miradi ya moja kwa moja na uunaleta ongezeko chanya kwenye uwezekezaji unaofanywa kupitia fedha za umma kwenye Sekta ya Kilimo.

Vile vile, kwa mwaka 2022/2023 Sekta binafsi imewekeza zaidi ya shilingi **1,807,481,862,772** katika Sekta ya Kilimo nchini ikiwa ni mwendelezo wa ongezeko chanya kiuwekezaji tangu kuanza kwa utekelezaji wa Programu mwaka 2018/2019. Pamoja na kuchangamkia fursa katika eneo la kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi; Sekta binafsi imeweza kuwekeza kwenye uongezaji tija kwa utumiaji wa mbegu bora, mbolea, teknolojia na zana za kisasa kwenye uzalishaji.

## Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023 Wizara za Kisekta

Eneo Kuu la Programu	Fedha za Ndani (Sh.)	Fedha za Nje (Sh)	Jumla (Sh.)	Asilimia ya mgawanyo
<b>Eneo la Kwanza:</b> Usimamizi na matumizi endelevu ya maji na ardhi	359,304,769,624	13,912,043,000	373,216,812,624	25
<b>Eneo la Pili:</b> Kuongeza Tija na Faida katika Kilimo	193,991,081,100	47,450,662,118	241,441,743,218	16
<b>Eneo la Tatu:</b> Biashara na Uongezaji Thamani kwenye Mazao	756,692,817,904	83,856,631,368	840,549,449,272	56
<b>Eneo la Nne:</b> Uwezeshi wa Sekta, Uratibu, Ufutiliaji na Tathmini	26,800,802,932	17,942,820,211	44,743,623,143	3
<b>Jumla Kuu</b>	<b>1,336,789,471,560</b>	<b>163,162,156,697</b>	<b>1,499,951,628,257</b>	100


### 2.0. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2022-2023

Katika mwaka 2022/2023 jumla ya shilingi **1,063,179,588,577** zilitolewa kwa ajili ya kutekeleza bajeti ya ASDP II kwenye maeneo yote makuu ya kupitia bajeti za Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine zinazotekeliza Programu (Jedwali Na. 2; Kiambatisho Na. 3). Kiasi hiki cha fedha zilizotolewa ni sawa na asilimia 71 ya kiasi cha fedha zilizotengwa ambapo takribani asilimia 98 ya fedha hizo zilizotoka ni fedha za ndani.

Aidha, kiasi cha Shilingi **1,048,748,551,694** zilitumika sawa na asilimia 99 ya fedha zilizotolewa ukiwa ni muendelezo mzuri wa utekelezaji wa programu kwa ujumla kwa miaka mitano ya Programu tangu mwaka 2018/2019 (Jedwali Na. 2; Kielelezo Na. 1; Kiambatisho Na. 4-5).

## Jedwali Na. 2: Utekelezaji wa Bajeti ya ASDP II Mwaka 2022/2023 Wizara za Taasisi za Kisekta

Eneo Kuu la Programu	Fedha zilizoidhinishwa			Fedha zilizotolewa			Asilimia (%) fedha ya zilizotolewa kati ya zilizotengwa	Fedha zilizotumika			Asilimia (%) ya zilizotumika kati ya zilizotolewa
	Fedha za Ndani (Shs)	Fedha za Nje (Shs)	Jumla (Shs)	Fedha za Ndani (Shs)	Fedha za Nje (Shs)	Jumla (Shs)		Fedha za Ndani (Shs)	Fedha za Nje (Shs)	Jumla (Shs)	
Eneo Kuu la Kwanza: Matumizi Endelevu ya Ardhi na Maji	359,304,769,624	13,912,043,000	373,216,812,624	196,146,971,340	1,508,634,149	197,655,605,489	52.96	195,103,898,274	1,508,634,149	196,612,532,423	99.47
Eneo Kuu la Pili: Kuongeza tija na Faida katika Kilimo	193,991,081,100	47,450,662,118	241,441,743,218	245,198,400,613	6,818,373,451	252,016,774,064	104.38	241,083,686,479	6,313,770,000	247,397,456,479	98.17
Eneo Kuu la Tatu: Biashara na Kuongeza Thamani	756,692,817,904	83,856,631,368	840,549,449,272	561,155,538,640	8,416,702,575	569,572,241,216	67.76	559,395,532,230	8,416,702,575	567,812,234,805	99.69
Eneo Kuu la Nne: Uwezesaji wa Sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini	26,800,802,932	17,942,820,211	44,743,623,143	38,685,441,528	5,249,526,281	43,934,967,809	98.19	36,079,836,479	846,491,507	36,926,327,986	84.05
<b>Jumla (Shs)</b>	<b>1,336,789,471,560</b>	<b>163,162,156,697</b>	<b>1,499,951,628,257</b>	<b>1,041,186,352,121</b>	<b>21,993,236,456</b>	<b>1,063,179,588,577</b>	<b>70.88</b>	<b>1,031,662,953,462</b>	<b>17,085,598,231</b>	<b>1,048,748,551,694</b>	<b>98.64</b>



### ***Kielelezo Na. 1: Utekelezaji wa Bajeti ya ASDP II Mwaka 2018/2019 hadi 2022/2023***

Aidha, miradi au kazi zipatazo 719 zilipangwa kutekelezwa kwenye maeneo yote makuu ambapo ni kazi 126 pekee sawa na asilimia 18 zilitekelezwa na kukamilika. Asilimia 53 ya kazi zilizopangwa hazikutekelezwa kwa sababu mbalimbali hususan kutopata fedha kama ilivyopangwa, pamoja sababu nyinginezo (Jedwali Na. 3; Kiambatisho Na. 7-11).

### **Jedwali Na. 3: Kiwango cha utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2022/2023**

<b>Eneo Kuu la Programu</b>	<b>Idadi ya Kazi</b>	<b>Kiwango cha Utekelezaji (%)</b>			
		<b>Kazi zisizotekelzwa</b>	<b>Kazi zilizotekelzwa kiasi</b>	<b>Kazi zilizokamilika</b>	<b>Jumla</b>
Matumizi Endelevu ya Ardhi na Maji	89	47	37	16	100
Kuungeza tija na faida kwenye kilimo, mifugo na uvuvi	247	51	27	22	100
Biashara na kuungeza thamani	119	66	22	12	100
Uwezeshaji Sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na tathmini	264	51	33	17	100
<b>Jumla Jumuishi %</b>	<b>719</b>	<b>53</b>	<b>29</b>	<b>18</b>	<b>100</b>

#### **2.1. Eneo Kuu la Kwanza: Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Ardhi na Maji na Ardhi**

Lengo la eneo hili ni kuhakikisha upatikanaji endelevu wa rasilimali maji na ardhi kwa ajili ya shughuli za uzalishaji wa mazao, mifugo na uvuvi

Katika kutekeleza Eneo Kuu la Kwanza la ASDP II, jumla ya Shilingi **373,216,812,624** zilipangwa katika bajeti za Wizara za Sekta ya Kilimo, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na asilimia 25 ya bajeti nzima ikiwa pia ni ongezeko kubwa la kibajeti lililotokana kutoa kipaumbele kwenye miradi ya umwagiliaji nchini ambapo jumla ya fedha zilizotolewa Shilingi **197,655,605,489** sawa na asilimia 53 ya fedha zilizotengwa. kati ya fedha zilizotolewa, Shilingi **196,612,532,423** zilitumika sawa na asilimia 99 ya fedha zilizotolewa (Jedwali Na. 1-2; Kiambatisho Na 2-5).

Kazi 89 zilipangwa kwenye Eneo Kuu la Matumizi Endelevu ya Ardhi na maji ambapo sehemu kubwa ya kazi zilizopangwa kwenye sekta ya mazao (66%) zilimetekelzwa (Jedwali 3-4; Kiambatisho 7-11). Zaidi ya nusu ya kazi zilizopangwa kwenye eneo hili zimetekelzwa.

### **Jedwali Na.4: Utekelezaji wa kazi kwenye Eneo Kuu la Kwanza Mwaka 2021/2022**

<b>Sekta Ndogo</b>	<b>Idadi ya Kazi</b>	<b>Kiwango cha Utekelezaji wa Kazi (%)</b>			
		<b>Haijatekelezwa</b>	<b>Imetekelzwa kiasi</b>	<b>Imekamilika</b>	<b>Jumla</b>
Mazao	42	33	45	21	100
Mifugo	12	58	42	0	100
Uvuvi	3	100	0	0	100
Mtambuka	32	59	25	16	100
	<b>89</b>	<b>48</b>	<b>36</b>	<b>16</b>	<b>100</b>

Kazi zilizofanyika na matokeo katika eneo kuu la matumizi endelevu ya ardhi na maji zililenga kwenye maeneo ya kipaumbele ya uwekezaji na baadhi ya kazi hizo ni kama ifuatavyo: -

#### 2.1.1 Mpango wa Matumizi ya ardhi na usimamizi wa mabwawa

- i. Ulipaji wa fidia ya kutwaa eneo lenye ukubwa wa hekta 160 kwa ajili ya uanzishwaji wa mashamba ya pamoja (block farms) eneo la Chinangali, Halmashauri ya Chamwino.
- ii. Hati za Hakimiliki za kimila zipatazo 51,764 zimetolewa katika mikoa mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Mbeya (22,225), Morogoro (5,771) na Singida (5,726).
- iii. Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 383 umefanyika katika halmashauri mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Makete DC (44), Ngorongoro DC (36), Meatu DC (28) na Korogwe DC (16).
- iv. Uandaaji wa mipangokina 11, Upimaji wa Viwanja (3,626) na Mashamba (1,604) katika eneo la Msomera Halmashauri ya Wilaya ya Handeni wanapohamishiwa kwa hiari wananchi kutoka Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro umefanyika;
- v. Kukamilika kwa kazi ya usanifu na uandaaji wa michoro kwa ajili ya ukaratabati wa mabwawa ya Ibadakuli- Shinyanga, Kilimatemb - Karatu, Ngamuriak- Monduli na Ngereiyan- Longido;
- vi. Kazi ya kuanzisha mpango wa usimamizi wa mazingira na kijamii (ESMP) katika umefanyika katika skimu 13 za umwagiliaji;

#### 2.1.2 Maendeleo ya Miundombinu ya Umwagiliaji

- i. Ufutiliaji wa ukarabati wa skimu mbili za umwagiliaji za Endagaw (Hanang) na Tlawi (Mbulu) umefanyika ambapo katika skimu ya Endagaw, kazi ya ukarabati imefanyika kwa asilimia 52.
- ii. Majaribio ya mfumo wa umwagiliaji kwa njia ya matone kwenye mashamba ya wakulima wadogo wa chai katika Wilaya za Rungwe, Njombe na Mufindi umefanyika
- iii. Kazi ya uhakiki wa Skimu na eneo linalomwagililwa imefanyika katika skimu 10 katika Mikoa ya Katavi, Tabora, Mbeya, na Morogoro.
- iv. Kukamilika kwa kazi ya usanifu na uandaaji wa michoro kwa ajili ya ukaratabati wa mabwawa ya Ibadakuli- Shinyanga, Kilimatemb - Karatu, Ngamuriak- Monduli na Ngereiyan- Longido;
- v. Ujenzi wa Skimu 14 za Uturo, Isenyela, Chosi, Herman, Mkombozi, Rudewa, Bonde la Eyasi, Membe, Kongogo, Rabour, Msingi, Illemba, Mahiga na Tlawi utekelezaji wake unaendelea;
- vi. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu ya Kilimi - Nzega (hekta 400), Arusha (hekta 200), Msimba (hekta 200) na Tengeru (hekta 10) unaendelea na umefikia asilimia 25. Aidha, uchimbaji wa visima virefu sita (6) katika shamba la mbegu la Msimba umefanyika;
- vii. Ujenzi wa mfereji wa umwagiliaji katika shamba la Malisho ya Mifugo Langwira inaendelea ambapo ujenzi wa mita 600 kati ya mita 2,000 za mfereji umekamilika;

### 2.1.3 Kuendeleza vyanzo vya maji kwa ajili ya mifugo na uvuvi

- i. Katika kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji katika maeneo ya Arusha, Monduli, Arumeru, Moshi Vijijini, Rombo, Same, Mwanga, Korogwe na Handeni, jumla ya vyanzo 10 kati ya 11 vimewekewa mipaka kwa kupanda beacons 3,500 na kupandwa miti rafiki kwa maji takriban 5,674.
- ii. Aidha, Jumuiya 11 za vidakio zimeimarishwa kwa kuzipatia elimu ya uoteshaji wa vitalu vya miti na vitendea kazi.

### 2.2. Eneo Kuu la Pili: Kuongeza Tija na Faida Katika Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Lengo la eneo kuu la pili la ASDP II ni kuongeza kiwango cha uzalishaji wenyе tija ambapo mkulima atatumia eneo na gharama ndogo kupata mavuno mengi zaidi. Aidha, ni eneo linalohakikisha upatikanaji na utumiaji wa chakula bora chenye viinilishe muhimu kwa maendeleo ya familia za wazalishaji na wananchi wote kwa ujumla.

Katika kutekeleza Eneo Kuu la Pili la Programu, jumla ya Shilingi **241,441,743,218** zilitengwa katika bajeti za Wizara za Sekta ya Kilimo, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kipindi cha mwaka 2022/2023. Katika kipindi hicho, Shilingi **252,016,774,064** zilitolewa ambazo ni sawa na asilimia 104 ya fedha zilizotengwa na kati ya hizo, Shilingi **247,397,456,479** zilitumika sawa na asilimia 98 ya zilizotolewa (Jedwali Na. 1-2; Kiambatisho Na.2-6).

Kazi 247 zilipangwa kufanyika kwenye Eneo Kuu la Kuongeza Tija na Faida kwenye kilimo, mifugo na uvuvi ambapo kazi 54 sawa na asilimia 22 ya kazi zilizopangwa zilitekelezwa kikamilifu (Jedwali 3; Jedwali Na. 5; Kiambatisho 7-11). Zaidi ya nusu ya kazi zilizopangwa katika eneo hili hazijatekelezwa kutokana na ukosefu wa fedha pamoja na sababu nyingine.

#### Jedwali Na.5: Utekelezaji wa kazi kwenye Eneo Kuu la Pili Mwaka 2022/2023

Sekta Ndogo	Idadi ya Kazi	Kiwango cha Utekelezaji wa Kazi (%)			
		Haijatekelezwa	Imetekelzwa Kiasi	Imekamilika	Jumla
Mazao	101	49	19	33	100
Mifugo	63	52	25	22	100
Uvuvi	35	57	29	14	100
Mtambuka	48	52	44	4	100
	<b>247</b>	<b>51</b>	<b>27</b>	<b>22</b>	<b>100</b>

Kazi zilizofanyika zililenga kwenye maeneo ya kipaumbele ya uwekezaji, na baadhi ya kazi hizo ni kama ifuatavyo;

#### **2.2.1. Kuimarisha huduma za ugani, mafunzo na uendelezaji wa huduma za taarifa**

- i. Maafisa ugani 203 wamefundishwa kuhusu kilimo biashara na matumizi ya mfumo wa M – Kilimo;
- ii. Ugharamiaji wa huduma ya chakula katika Vyuo 14 vya Mafunzo ya Kilimo nchini ambapo wanafunzi 3,151 wamedahiliwa kwa ngazi ya Astashahada na shahada katika mwaka wa masomo 2022/2023;
- iii. Kazi ya ujenzi wa maboma ya kumbi mbili za mihadhara zenyne uwezo wa kuchukua wanafunzi 240 kila mmoja zimeanza kwa kampasi mbili za Mpwapwa na Morogoro na ujenzi huo umefikia asilimia 40 kwa kampasi zote mbili;
- iv. Ununuzi wa pipipiki 3,500 na kuzisambaza katika mikoa 15 ambayo ni Morogoro, Iringa, Mbeya, Rukwa, Songwe, Mtwara, Lindi, Mara, Shinyanga, Mwanza, Geta, Kagera, Kigoma, Tanga na Pwani umefanyika;
- v. Maafisa ugani 417 kutoka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wamepata mafunzo kuhusu teknolojia za uzalishaji mifugo;
- vi. Jumla ya Maafisa ugani 387 kutoka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za mitaa wamepata mafunzo kuhusu teknolojia za uzalishaji mifugo;
- vii. Jumla ya mashamba darasa 98 ya malisho ya mifugo yamepandwa malisho katika Halmashauri 44;
- viii. Uandaaji na uendeshaji wa mashamba ya maonesho 82 umefanyika katika Halmashauri ya Korogwe Mji mashamba (31), Kinondoni Mamispaa mashamba (14), Iringa MC (4), Kilolo DC (7) na Geita Mji (26);
- ix. Kuwezesha Maafisa Ugani 400 katika fani za Mazao, Mifugo na Uvubi kupatiwa vitendea kazi vya kutolea huduma za ugani (extension gears/kits kits n.k) katika Halmashauri 12;

#### **2.2.2. Utafiti na maendeleo**

- i. Ukarabati na kuzipatia vifaa na vitendanishi maabara 3 za TARI Mlingano (Maabara udongo na maabara ya tissue culture) na TARI Mikocheni (maabara ya GMO);
- ii. Utafiti na uzalishaji wa mbegu bora za alizeti umefanyika;
- iii. Utafiti wa magonjwa mbali mbali ya mifugo 125,000 umefanyika katika Halmashauri ya Manyoni DC;
- iv. Kazi ya utafiti wa uwangi, bioanuwai na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika imekamilika. Aidha, matokeo ya utafiti yamebainisha kwamba kuna kushuka kwa wingi wa samaki kutoka tani 157,493 mwaka 1995 hadi tani 144,690 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 8;

#### **2.2.3. Upatikanaji bora wa pembejeo na huduma za afya ya mazao, mifugo na uvubi**

- i. Ujenzi wa majosho 253 unaendelea kwenye mikoa mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Katavi (22), Simiyu (23), Manyara (32), Morogoro (13) na Mwanza (11) na Tanga (10) ambapo ujenzi umefikia wastani wa asilimia 80. Aidha, lita 22,000 za dawa ya kuogesha mifugo zimenunuliwa;

- ii. Hereni 150,000, vichochea joto (hormones) na vifaa vingine vimenunuliwa kwa ajili ya utambuzi wa ng'ombe wanaohimilishwa katika kambi ili kufuatilia kiwango cha ushikaji mimba na kutambua mbari za mifugo zilizozaliwa. Ng'ombe 14,711 wamehimilishwa.
- iii. Uzalishaji wa mbegu bora za chikichi umeendelea ambapo kilo 2,130,000 zimezalishwa. Kati ya hizo, mbegu kilo 1,580,000 zimesambazwa katika Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Magereza, ASA na Halmashauri za Mikoa 9 kwa ajili ya uoteshaji.
- iv. Jumla ya sampuli 481 kutoka kwenye mafungu ya mbegu (Seed Lots) yenyе uzito wa tani 7,309.8 zimefanyiwa vipimo vya maabara. Kati ya sampuli zilizofanyiwa vipimo hivyo, sampuli 481 (86.3%) zilifaalu wakati sampuli 32 (6.6%) hazikufaulu na sampuli 34 (7.1%) ziliwu zinaendelea kufanyiwa vipimo vya maabara.
- v. Usajili wa wafanyabiashara ya mbegu wapatao 106 umefanyika, kati ya hao wenye makampuni ni 10, wauzaji wa mbegu ni 85 na wakulima wadogo wa mbegu za QDS;
- vi. Ununuzi na usambazaji wa lita 60,000 za viuatilifu katika Halmashauri 55 za Mikoa ya Manyara, Singida, Tabora, Katavi, Tanga, Geita, Simiyu, Shinyanga, Ruvuma, Kilimanjaro, Arusha na Dodoma na kudhibiti milipuko ya viwavijeshi na kuweza kuokoa hekta 110,000 za mazao ya wakulima. Vilevile, kilo 2,000 za viuatilifu zimetumika kudhibiti panya katika mikoa ya Morogoro, Mtwara na Lindi pamoja na lita 300 kwa ajili ya kudhibiti nzi wa matunda katika mikoa ya Tanga, Dar es Salaam na Mwanza;
- vii. Tani 90.764 za mbegu za korosho zimesambazwa katika Halmashauri 86 ambazo zitazalisha miche 12,706,960;
- viii. Wakala wadogo wa Wakulima Wadogo wa Chai -(TSHTDA) wamevezeshwa na wamezalisha miche 721,000 ya chai;
- ix. Miche bora ya kahawa 8,784,146 imezalishwa na kusambazwa ikiwa sawa na asilima 43.9 ya lengo la kuzalisha miche 20,000,000.

#### **2.2.4. Kuimarisha na kukuza uchumi wa kilimo (mazao, mifugo na Uvuvi)**

- i. Jumla ya boti 78 kati ya boti 158 sawa na asilimia 49 zimeshatengenezwa na mkandarasi anaendelea na utengenezaji wa boti zilizobaki kwa ajili ya kuongeza tija kwenye shughuli za uvuvi nchini. Aidha, mchanganuo wa boti zilizotengenezwa ni kama zifuatazo; - boti 40 zenyе ukubwa wa mita 8; boti 28 zenyе ukubwa wa mita 5; boti 3 zenyе ukubwa wa mita 10; boti 4 zenyе ukubwa wa mita 12; na boti 3 zenyе ukubwa wa mita 14 zimetengenezwa.
- ii. Mbuzi 1780 aina ya Malya wamenunuliwa na kusambazwa kwa wananchi kwa ajili ya kuwasaidia kujikwamua kiuchumi. Aidha, madume 366 yamenunuliwa na kusambazwa kwa wafugaji kupitia vikundi vya Wafugaji katika Halmashauri nane (8) za Chamwino (50), Msalala (50), Maswa (50) na Chato (50), Buchosa (36), Mvomero (40), Mkuranga (40) na Mkalama (50). Vilevile, Ununuzi wa ng'ombe 7200 wa kunenepesha katika vituo vya Mabuki, Tanga na Kikulula umefanyika ikiwa ni pamoja na kununua vyakula ziada vya mifugo hiyo;
- iii. Umefanyika upanuzi wa vituo vya ukuzaji viumbe maji vya Ruhila - Songea (ujenzi wa jengo la kutotoleshea vifaranga umefikia hatua ya kuezeka) na Nyengedi - Lindi (ujenzi wa jengo la kutotoleshea vifaranga na ofisi umefikia hatua ya kumwaga jamvi la msingi); Ruvula - Mtwara (Ujenzi wa kuta za jengo la kitotoleshi na maabara

umekamilika na mkadarasi anaendelea na kazi ya kuezeka, kuweka za madirisha na milango ya jengo, ujenzi wa matanki 15 ya kuzalishia vifaranga, na mnara wa maji umekamilika)

### **2.3. Eneo Kuu la Tatu: Biashara na Kuongeza thamani ya mazao**

Eneo hili lina lenga kutatua vikwazo vyta upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa wakulima na kuongeza thamani ya mazao. Hii ni pamoja na: (i) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika kilimo-biashara; (ii) Kuboresha mifumo ya kudumu ya masoko (iii) Kuboresha miundombinu ya masoko ikiwemo barabara za vijijini na maghala (iv) Upatikanaji wa taarifa za uhakika za masoko (v) Kuhamasisha usindikaji na uongezaji wa thamani katika mazao.

Katika kutekeleza Eneo Kuu la Tatu la ASDP II, jumla ya **Shilingi 840,549,449,272** zilitengwa katika bajeti za Wizara za Sekta ya Kilimo, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha Mwaka 2022/2023. Fedha zilizotolewa katika kipindi hicho ni **Shilingi 569,572,241,216** sawa na asilimia 68 ya fedha zilizopangwa. Aidha, kati ya fedha zilizotolewa, **Shilingi 567,812,234,805** zilitumika sawa na asilimia 99 ya fedha zilizotolewa.

#### **Jedwali Na.6: Utekelezaji wa kazi kwenye Eneo Kuu la Tatu Mwaka 2022/2023**

Sekta Ndogo	Idadi ya Kazi	Kiwango cha Utekelezaji wa Kazi (%)			
		Haijatekelezwa	Imetekelzwa kiasi	Imekamilika	Jumla
Mazao	39	67	26	8	100
Mifugo	33	76	21	3	100
Uvuvi	15	87	7	7	100
Mtambuka	32	47	25	28	100
	<b>119</b>	<b>66</b>	<b>22</b>	<b>12</b>	<b>100</b>

Jumla ya kazi 119 zilipangwa kufanya kazi kwenye Eneo Kuu la Biashara na Kuongeza Thamani ya katika kilimo, mifugo na uvuvi ambapo kazi zipatazo 40 pekee ziliweza kupata fedha na kutekelezwa ikiwa ni sawa na asilimia 34 ya kazi zote. Sehemu kubwa ya kazi kwenye eneo hili hazikutekelezwa licha ya kuwa ni eneo linalopata fedha nyingi kuliko maeneo yote, hii inatokana na kazi za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara za vijijini kuwa na thamani kubwa zaidi kifedha licha ya namba (idadi) ndogo ya kazi (Jedwali 1- 3; Jedwali Na. 6; Kiambatisho 6-11).

Kazi zilizofanya kazi zililenga kwenye maeneo ya kipaumbele ya uwekezaji. Baadhi ya kazi hizo ni kama ifuatavyo;

#### **2.3.1. Kuendeleza upatikanaji wa soko kwa bidhaa zote za kipaumbele**

- i. Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) ilinunua Mahindi tani 3,038 kutoka kwa wakulima wadogowadogo na vyama vyta wakulima AMCOS kwa gharama ya

- shilingi 1,822,800,000. Gharama za manunuzi zilizotumika ni asilimia 6.45 ya jumla ya manunuzi ambapo gharama hizo zina jumla ya shilingi 117,490,000.
- ii. Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (National Food Reserve Agency-NFRA) imenunua tani 18,294.314 za chakula. Kati ya hizo, tani 17,257.857 ni za mahindi na tani 1,036.457 ni za mtama. Aidha, kiasi kilichonunuliwa kikijumuishwa na bakaa ya tani 141,575.902 kinafanya NFRA kuhifadhi jumla ya tani 159,870.216 katika ghala zake.
  - iii. Barabara zenyе utrefu wa Kilomita 8,583.04, mifereji ya kuondoa maji barabarani 14,392.04m na boksi kalvati 14 zimetengenezwa ili kurahisisha ufikiaji wa masoko na huduma za pembejeo za uzalishaji. Hii ni pamoja na ujenzi wa 3.9 Km za barabara za mashambani (Feeder/access road) katika Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam.

### **2.3.2. Maendeleo ya biashara za kilimo, Miundombinu ya kuongeza thamani na usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo na Uvuvi**

- i. Kuwezesha ujenzi wa masoko ya mazao ya kilimo mawili katika Halmashauri ya Rombo DC;
- ii. Kuwezesha ujenzi wa masoko mawili ya mifugo katika Halmashauri za Uvinza na Momba;
- iii. Ujenzi wa machinjio za kati (slaughter houses) mbili za mifugo katika Halmashauri ya Kigoma Ujiji na Mafinga TC;
- iv. Kuwezesha ukarabati wa machinjio 4 ya mifugo (slaughter slabs) katika Halmashauri za ileje (1), Njombe TC (1) na kyela (2);
- v. Kuwezesha ujenzi wa ghala 2 za kuhifadhia mazao katika Halmashauri ya Moshi DC (1) na Njombe DC (1);
- vi. Mkataba wa ujenzi wa ghala 28 kati ya 70 umesainiwa na wakandarasi wamekabidhiwa maeneo ya jenzi kwa ajili ya kuanza kazi. Aidha, kutokana na kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi na usafirishaji jumla ya ghala 38 kati 70 zimepangwa kujengwa;
- vii. Kukamilika kwa ukarabati wa ghala mbili (2) za mazao za Litisha na Lilondo B. Aidha, ukarabati wa ghala (5) za Litisha, Lipaya, Liula, kizuka, Hangangadinda na Lilondo A unaendelea;
- viii. Kukamilika ujenzi wa vihenge 20 umekamiliki katika mji wa Babati (8), Sumbawanga (6), na Mpanda (6)
- ix. Kukamilika kwa ujenzi wa ghala 4 katika mji wa Babati (2), Sumbawanga (1), Mpanda (1).

### **2.4. Eneo kuu la Nne: Uwezeshaji wa Sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini**

Eneo hili linalenga kuweka mazingira wezeshi ya Sekta ya kilimo, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini. Hii ni pamoja na: (i) Kupitia sera na miongozo inayoweka mazingira wezeshi ya biashara kwenye sekta ya kilimo; (ii) Kuboresha na kuimarisha uratibu wa sekta; (iii) Kuimarisha mifumo ya tathmini na ufuatiliaji wa Sekta ya kilimo; (iv) Kuboresha uwezo na mifumo ya ukusanyaji na usimamizi wa takwimu za kilimo; (v) Kujenga uwezo katika ngazi zote; (vi) Kuboresha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa ajili ya Kilimo; (vii) Kuimarisha huduma za Kifedha; na (viii) Kuimarisha ushiriki wa jinsi zote kwenye shughuli za kilimo.

Katika kutekeleza Eneo Kuu la Nne la ASDP II, jumla ya Shilingi **44,743,623,143** zilitengwa katika bajeti za Wizara za Sekta ya Kilimo, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kipindi cha mwaka 2022/2023. Katika kipindi hicho, shilingi **43,934,967,809** zilitolewa sawa na asilimia 98 ya fedha zilizopangwa. Aidha, katika kipindi hicho, shilingi **36,926,327,986** zilitumika sawa na asilimia **84** ya fedha zilizotolewa (Jedwali Na. 1-2; Kiambatisho Na. 2-6).

#### **Jedwali Na.7: Utekelezaji wa kazi kwenye Eneo Kuu la Nne Mwaka 2021/2022**

<b>Sekta Ndogo</b>	<b>Idadi ya Kazi</b>	<b>Kiwango cha Utekelezaji wa Kazi (%)</b>			
		<b>Haijatekelezwa</b>	<b>Imetekelawa kiasi</b>	<b>Imekamilika</b>	<b>Jumla</b>
Mazao	65	48	32	20	100
Mifugo	28	57	36	7	100
Uvuvi	25	60	32	8	100
Mtambuka	146	49	32	18	100
	<b>264</b>	<b>51</b>	<b>33</b>	<b>17</b>	<b>100</b>

Jumla ya kazi 264 ilipangwa kufanyika kwenye Eneo Kuu hili ambapo miradi/kazi 44 sawa na asilimia 19 ya kazi zilizopangwa zilitekelezwa kikamilifu (Jedwali 3; Jedwali 7 na Kiambatisho 6-11). Kazi zilizofanyika zililenga kwenye maeneo ya kipaumbele ya uwekezaji ambapo baadhi ya hizo ni kama ifuatavyo;

#### **2.4.1. Sera na Mfumo wa udhibiti na Maendeleo ya Mazingira ya Biashara**

- i. Mkutano wa wadau wa mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ulifanyika Jijini Dodoma ambapo jumla ya wadau 35 kutoka Sekretarieti ya Mikoa na Mamlaka ya Serikali za mitaa walishiriki;
- ii. Sheria ya Biashara ya Ngozi Na.18 ya mwaka 2010 imefanyiwa mapitio kwa ajili ya uboreshaji

#### **2.4.2. Kuimarisha uwezo wa taasisi na wa kiufundi wa wazalishaji wadogo waliopo na wapya, biashara na vikundi vya wakulima wa usindikaji na vyama vya ushirika**

- i. Ukaguzi (Inspection) umefanyika wa maduka ya pembejeo za Kilimo katika Halmashauri 13 za Makambako TC, Njombe TC, Kibaha TC;
- ii. Ukaguzi umefanyika katika mdauka 97 ya Halmashauri za Njombe DC, Makambako TC na Njombe Mji;
- iii. Ukaguzi umefanyika (Inspection) wa maduka 58 ya pembejeo za Kilimo katika Halmashauri Mji Tunduma;
- iv. Kuwezesha ukaguzi (Inspection) wa maduka ya Vyakula vya Mifugo, Viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo na machinjio, Vituo vya afya ya mifugo, masoko ya mifugo, mabucha katika Halmashauri 2 za Kibaha Mji na Lushoto;

- v. Kuwezesha Uanzishaji na Usajili wa Vyama vya Ushirika (AMCOs) 4 katika Halmashauri 1 ya Ikungi DC; na
- vi. Ukaguzi wa mahesabu ya vyama vya Ushirika 13 ulifanyika katika Halmashauri ya Makambako.

#### **2.4.3. Kuboresha na kuimarisha uratibu kati ya Wizara za Kisekta na Wadau**

- i. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023 Kitengo cha Uratibu wa Programu, Kiliratibu vikao saba (7) vya timu ya Waratibu wa Wizara na Taasisi za Kisekta (NACOTE), vikao vinne (4) vya Wakurugenzi (TCD) na Kikao kimoja cha Kundi la Ushauri wa Kisekta.
- ii. Shughuli za awali za utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi (AFDP) zimeanza kutekelezwa ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vitendea kazi kama magari, kompyuta na samani umefanyika;
- iii. Mkutano wa wadau wa Kilimo umefanyika ukijumuisha takribani wadau 50 uliofanywa sambamba na uzinduzi wa kilimo cha mashamba makubwa (block farming);

#### **2.4.4. Kuendeleza mfumo wa ufuatiliaji na tathmini katika sekta ya kilimo**

- i. Imefanyika tathmini ya uharibifu wa mazao ya kilimo kutohana na mvua ya mawe katika kijiji cha Bukoli pamoja na kutoa chakula cha msaada kwa wahanga kupitia mgodi wa Bacleef;
- ii. Tathmini ya kiutendaji ya vyama vya wamwagiliaji imefanyika katika skimu 12 katika Mkoa wa Morogoro;
- iii. Ufuatiliaji na tathmini pamoja na usimamizi wa shughuli zilizotekelawa na Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika Halmashauri 8 za Korogwe DC, Handeni TC, Handeni DC, Manyoni, Singida MC, Buhigwe DC, Kalambo DC, Nkasi DC, Makete DC, Njombe DC umefanyika;
- iv. Ufuatiliaji umeafanyika kwa Skimu za Mgongola (Mvomero), Rudewa (Kilosa), Ulyanyama (Sikunge), Idudumo (Nzega), Goweko (Tabora), Mgambalenga (Kilolo), Mkombozi, Luganga, Muhukuru, Chosi, Herman, Uturo, Isenyela, Mseseule na Matebete;
- v. Ukaguzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji katika Skimu 13 umefanyika;
- vi. Skimu 4 zimefanyiwa ufuatiliaji katika Halmashauri za Mvomero (Mgongola na Lukenge), Kilosa (Rudewa) na Mlimba (Idete); na
- vii. Ufuatiliaji wa usajili wa wakulima umefanyika katika Halmashauri 9 za Mkoa wa Morogoro ambapo jumla ya vitabu 1,671 vimesambazwa na wakulima 86,263 wamesajiliwa. Kufuatilia hali ya chakula na mwenendo wa bei za mazao umefanyika kwa Halmashauri zote ambapo bei imeonekana kupanda lakini chakula kinatosheleza.

#### **2.4.5. Upatikanaji wa mikopo, huduma za kifedha na bima**

Upatikani wa mikopo kwenye Sekta ya Kilimo imeendelea kuimarika nchini ambapo kwa mwaka 2022/2023 jumla ya shilingi **1,807,481,862,772** zilitolewa na taasisi za kifedha hususan benki ya CRDB, NMB, TADB, NBC, TIB na Mfuko wa Pembejeo (Jedwali Na. 8).

#### **Jedwali Na. 8: Kiasi cha Mkopo uliotolewa na Taasisi za Kifedha\***

Sekta Ndogo	Orodha ya Taasisi za Kifedha na kiasi cha mkopo kilichotolewa					Jumla (Shs)
	TADB	CRDB	AGITF	NMB	TIB	
Kilimo-Mazao	121,226,087,798	1,258,536,600,836	-	225,419,214,696	2,531,425,876	1,607,713,329,205
Mifugo	27,843,220,981	22,808,646,598	-	33,190,024,800	320,876,158	84,162,768,537
Uvvi	2,617,845,050	19,223,609,123	-	-	-	21,841,454,173
Misitu na Nyuki	-	18,789,964,535	-	900,000,000	-	19,689,964,535
Kilimo Mchanganyiko	-	69,652,060,067	1,371,400,000	3,050,886,255	-	74,074,346,322
	<b>151,687,153,828</b>	<b>1,389,010,881,159</b>	<b>1,371,400,000</b>	<b>262,560,125,751</b>	<b>2,852,302,034</b>	<b>1,807,481,862,772</b>

\*Mkopo uliotolewa kwa taasisi binafsi

Serikali inaendelea kushirikiana na wadau wa bima kuandaa mpango mahsus wa bima ya kilimo nchini (Tanzania Agricultural Insurance Scheme). Hata hivyo baadhi ya Taasisi zimeendelea kutoa huduma ya bima ya mazao kwenye sehemu mbalimbali nchini.

Katika mwaka 2022/2023, Shirika la Bima la Taifa (National Insurance Corporation - NIC), Jubilee Insurance, MGen Insurance, Reliance Insurance, na Acre Africa Limited wameendelea kutoa huduma za bima ya mazao kwa wakulima. Hadi Juni 2023, NIC imetoa huduma ya bima ya mazao kwa wakulima wa mpunga 1500 katika mkoa wa Mbeya, Songwe na Katavi; wakulima wa Tumbaku 4540 wa katika mkoa wa Mbeya, Tabora na Shinyanga;

Aidha kampuni ya bima ya MGen imetoa huduma ya bima ya mazao kwa wakulima 243 wenye jumla ya ekari 714 kwa mazao mbalimbali ikiwemo: mahindi, mpunga, nyanya, ufuta, kahawa, korosho na Chai. Katika kipindi hicho, MGen wamefanya mafunzo kwa wakulima 2,520 wa vyama vya ushirika vya Marambo Amcos, Ngunichile Amcos, Mtua Amcos, Mbondo Amcos, Kitandi Amcos, Asema Amcos, Nguvumali Amcos, Mwampuli amcos. Vyama hivyo viro katika mikao ya Katavi, Dodoma, Mtwara, Ruvuma na Mbeya;

Jubilee Allianz Tanzania imetoa huduma ya bima ya mazao kwa AMCOS 24 zenyé jumla ya wakulima 3,383 katika msimu wa 2021/2022. Kati ya hao, wakulima 2,721 wa zao la tumbaku katika mikao ya Shinyanga, Mbeya na Tabora na wakulima 662 ni wa zao la alizeti mkoani Singida.


Reliance Insurance inatoa huduma ya bima ya zao la mtama mweupe (white sorghum) kwa kampuni ya Kibaigwa Flour Supplies (KFS) mradi wa kampuni ya Bia TBL; na

Acre Africa, ni Kampuni inayofanya kazi kwa kushirikiana na kampuni za bima kuandaa bidhaa mbalimbali za bima. Katika mwaka wa fedha wa 2022/23, Acre Africa imeshirikiana na: NMB

Bank, NBC Bank, CRDB Bank, Azania Bank, mitando ya Simu katika kuandaa na kutoa bidhaa za bima za kilimo ambazo zimenufaisha zaidi ya wakulima 100,000 katika mikoa Zaidi ya 10 Tanzania. Aidha ACRE Tanzania, inatarajia kuzindua huduma ya bima ya Mifugo (Livestock Insurance) kwa jamii ya wafugaji nchini ambayo inatarajia kunufaisha wakulima zaidi ya 30,000 katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Arusha, Manyara, Kagera na Kilimanjaro.


### **3.0. USHIRIKI WA WASHIRIKA WA MAENDELEO:**

Mbali na uchangiaji wa Washirika wa Maendeleo (DPs) kwenye utekelezaji wa bajeti ya ASDP II kupitia bajeti za Wizara na Taasisi za Sekta ya Kilimo ambaa ulikuwa ni takriban shilingi 163,162,156,697 (Jedwali Na.1-2) ambapo wadau ikiwemo Benki ya Dunia (WB), Jumuiya ya Ulaya (EU) wamekuwa ni sehemu ya kubwa ya uchangiaji huo. Hata, hivyo, kiwango cha uchangiaji kwenye bajeti kimekuwa ukishuka mwaka hadi mwaka ambapo kwa mwaka 2022/2023 ni asilimia 11 (Kielelezo Na. 2; Kiambatisho Na. 12).



**Kielelezo Na. 2: Kiwango cha Fedha za Nje kwenye Bajeti ya Sekta ya Kilimo**

Kiasi kikubwa cha mchango wa Washirika wa Maendeleo unapitia miradi ya moja kwa moja (Direct Financed/Standalone Projects) kwa mwaka 2022/23 miradi ipatayo 73 yenye thamani ya takribani **Shilingi 314,502,359,204.94** iliorodheshwa wadau na hivyo kuongeza wigo thamani ya uwekezaji unaofanywa na umma kwa mwaka (annual public investment) kwenye maeneo yote makuu ya Programu (Jedwali Na. 9; Kielelezo Na. 3).



### **Kielelezo Na. 3: Bajeti ya Utakelezaji wa ASDP II na Ujumuishi wa Miradi ya Moja kwa Moja**

Eneo kuu la pili ambalo lina idadi kubwa zaidi ya miradi likichangizwa na miradi ya tafiti kuitia Taasisi za CGIAR (Consortium Group International Agricultural Research) (Jedwali Na. 9; Kiambatisho 12).

Taasisi nyingine zenyetmiradi ya moja kwa moja ni pamoja na Jumuiya ya Ulaya (EU), Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), Programu ya Chakula Duniani (WFP), Shirika la Wanawake (UN-Women), Ubalozi wa Ufaransa na Taasisi ya Maendeleo ya Ufaransa (FAD), Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Ubalozi wa Uhlanzi, Ubelgiji, Norway na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA).

### **Jedwali Na. 9: Miradi ya moja kwa moja ya Washirika wa Maendeleo Mwaka 2022**

Na	Eneo Kuu la Program	Idadi ya Miradi	Fedha zilizotengwa (Tsh)
1	Usimamizi na Matumizi Endelevu ya Ardhi na Maji	9	25,692,711,936.00
2	Kuongeza Tija na Faida kwenye Kilimo, Mifugo na Uvubi	35	120,389,072,361.20
3	Biashara na Kuongeza Thamani ya Mazao	7	61,007,971,253.33
4	Uwezeshi wa Sekta, Uratibu, Tathmini na Ufuatiliaji	22	107,412,603,654.41
	<b>Jumla</b>	<b>73</b>	<b>314,502,359,204.94</b>

#### 4.0. USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI

Sekta Binafsi ina mchango mkubwa katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara nchini ikiwa ni pamoja na malighafi za viwanda. Karibu asilimia 97 ya uzalishaji kwenye kilimo, mifugo na uvuvi ni matokeo ya uwekezaji Sekta Binafsi unaotekelawa wazalishaji wadogo wadogo (Jedwali Na. 10).

#### Jedwali Na. 10: Mlinganyo wa uzalishaji wa baadhi ya mazao katika Sekta Binafsi

